

## **Idara ya Utumishi na Utawala.**

Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto ina jumla ya Idara (13) na Vitengo sita (6). Kuna Tarafa saba (7), Kata ishirini na tatu (23), Vijiji sitini na tatu (63) na Vitongoji mia mbili themanini na moja (281).

Kimsingi Idara ya Utumishi na Utawala katika kutekeleza majumu yake inazingatia misingi ya utawala bora katika kutoa huduma bora kwa watumishi na jamii kwa ujumla.

### **Majukumu ya Idara:-**

- i. *Kuandaa bajeti ya mishahara na ikama ya watumishi.*
- ii. *Kutafsiri na kushughulikia miundo ya Utumishi.*
- iii. *Kuajiri kwa kuomba vibali vya ajira Utumishi Makao Makuu.*
- iv. *Kupandisha vyeo na kuthibitisha watumishi kazini.*
- v. *Kusimamia na kushughulikia maadili na nidhamu za watumishi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo.*
- vi. *Kusimamia na kuhakikisha vikao na mikutano yote ya kisheri na kikanuni Kata ngazi zote inafanyika.*
- vii. *Kuandaa na kusimamia mpango wa mafunzo kwa watumishi wakiwa nje na ndani ya vituo vya kazi.*
- viii. *Kushughulikia mafunzo ya kuwajengea uwezo Watumishi, Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa.*
- ix. *Kutathimini utendaji kazi wa watumishi.*
- x. *Kushughulikia mambo ya itifaki kwa watumishi.*
- xi. *Kufanya ukaguzi wa Payroll ya mishahara kwa kwa kushirikiana na wakuu wa Idara kila mwexi na kutolea taarifa iwapo kutakuwa na mapungufu au usahihii wa payroll husika.*
- xii. *Kuhakikisha watumishi wote ambao muda wao umefikia ukomo kwa sababu mbali mbali wanaondolewa katika payroll kupitia Mfumo wa LAWSON.*

- xiii. Kuandaa Tange kwa kila robo ya mwaka na mwaka mzima.*
- xiv. Kutafsiri sheria, kanuni na nyaraka mbali mbali za Serikali katika utumishi wa umma.*
- xv. Kutekeleza miongozo na mazoezi ya kitaifa yanayo tolewa.*
- xvi. Kusimamia ulinzi na usalama wa mali zote za Halmashauri.*
- xvii. Kushughulikia haki na stahiki za watumishi*
- xviii. Kusimamia Mifumo ya usafiri wa magari ya Halmashauri.*
- xix. Kushirikiana na Taasisi zingine katika masuala mbalimbali ya kiutendaji.*

### **Uhakiki wa Watumishi**

Kuanzia mwezi wa Machi 2016 Idara imetekeleza zoezi la uhakiki wa watumishi hewa pamoja na uhakiki wa vyeti vya watumishi na sasa bado tunaendelea na zoezi la uhakiki kila mwezi kabla ya kulipa mishahara.

### **Mafunzo**

Pia Idara kwa kutumia fedha za LGDG kwa mwaka wa fedha 2016/2017 yametolewa mafunzo kwa Waheshimiwa Madiwani kuhusu utawala bora, na Wakuu wa Idara na Vitengo nao walipata mafunzo yanayohusu Usambazaji wa Miongozo ya Mfumo wa Utekelezaji wa Fedha za Maendeleo Kwenye MSM (LGDG) iliyoboreshwa.